**Title: Under the Mango Trees**

**EPISODE 4**

**Author: Romie Singh**

**Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun**

**List of characters for episode 4:**

- Narrator
- Desirée
- Lorraine
- Eric
- Bongo

**INTRO**

Karibu kwenye sehemu ya nne katika mfululizo wa mchezo wa redio katika Noa Bongo Jenga maisha Yako. Leo hii katika kisa cha Chini ya Miembe tutazingatia mpango wa uzazi na jinsi watu hususan vijana wanavyoweza kujikinga na mimba zisizo takikana, Virusi vya HIV na maambukizo ya magonjwa ya zinaa. Tutaangazia pia njia mbali mbali za mpango wa uzazi. Leo, Desirée agundua tembe za aina Fulani chumbani kwa Lorraine na Eric anahisi kuwa anavutiwa na Desirée.

**Short music break**

**NARRATOR:** Jioni nzima Desirée alijifunza wimbo ambao yeye na rafiki yake Lorraine wangemuimbia Bongo siku inayofuata.hakuamini kama

angeweza kuwa na rafiki kama Lorraine na pia kuja kumtembelea katika nyumba yao nzuri mjini Kentown. Wasichana hawa wawili wanatoka kwenye hali tofauti kabisa kimaisha lakini wanaelewana vyema. Wote wanapenda kuimba au kurap. Lakini jioni ile DESIRÉE angegundua jambo geni kabisa kuhusu rafiki yake mpendwa.

**Sc. 1 In the bedroom. Lorraine and Desirée are practicing a new song.**

1. **SFX:** FADE IN ON SINGING AND LAUGHING

2. LORRAINE: haya sasa tuvae tujipambe! Hebu fungua droo, Des. Utaona skafu ya manyoya ya rangi ya pinki, ivae! **(giggling)** na mimi nitavaa hii kofia!

3. **SFX:** Drawer opening

4. DESIRÉE: Oh! Na hizi ni nini? Tembe?

5. LORRAINE: Whoops. Ssmshsni. Nimesahau kuwa ziko hapo. Hukupaswa kuziona.

6. DESIRÉE: Kwa nini?kwani ni za nini?

7. LORRAINE: Hivyo ni vijitembe.

8. DESIRÉE: Eti nini – Ni tembe za kupanga uzazi?

| | | |
|---|---|---|
| 9. | LORRAINE: (lovingly) | Ndio. sikiliza, Des, unamjua Sazi? |
| 10. | DESIRÉE: | namjua sana. Uko naye kwa muda mrefu. |
| 11. | LORRAINE: | Wajua, mimi na yeye … wajua tena... |
| 12. | DESIRÉE: | Hapana, sijui. Alaa? Una maana kuwa nyinyi mnafanya mapenzi? |
| 13. | LORRAINE: | Ndio! Usishangae. Hata dada yako,Bella anafanya mapenzi! Des – sisi tuna umri wa miaka18! Tuna weza kupiga kura na hata kuolewa. |
| 14. | DESIREE: | lakini sikufikiria kama wewe na Sazi... mna uhusiano wa karibu hivyo. |
| 15. | LORRAINE: | Oh, samahani sikukueleza mapema. Mimi ni mkubwa kwako kwa miaka miwili, Des – hatuko darasa moja. Hamna neno mradi sasa umejua. |
| 16. | DESIRÉE: | Ndio. Nimejua, kwa hivyo? Tembe hizi zinafanya kazi hasa? |
| 17. | LORRAINE: | Kwa ufupi, tembe hizi zinazuia kupata mimba. Tazama – hata paketi zinaeleza. |

Tembe zina kiasi kidogo cha Homoni kinacho zuia rutuba.

18. DESIRÉE: Zinakufanya ujisikie vipi?

19. LORRAINE: Barabara! Sipati damu nyingi sana wakati wa hedhi na ninaweza kuimba hata kucheza kwenye jukwaa wakati wowote ule ninapotaka. Yaani niko huru wakati wowote!

20. DESIRÉE: Jamani si hatari hiyo?

21. LORRAINE: Nafikiri kupata mimba ni hatari kubwa! Tembe ni salama na inafanya kazi yake sawa sawa. Hatari kubwa ni pale utakaposahau kuimeza. Lazima nimeze tembe moja kila siku tena kwa wakati ule ule.Nikikosa siku moja tu basi ninaweza kupata mimba.

22. DESIRÉE: (thoughtful) Na ulijuwaje juu ya tembe hizi?

23. LORRAINE: Unajua , mama yangu anafanya kazi kwenye kliniki ya kina mama wazazi. Yeye ni mshauri wa mambo ya kupanga uzazi.

24. DESIRÉE: (disbelief) Mama yako? Yaani Aunty Alice amekusaidia?

25. LORRAINE: (laughing) Angalia sura yako! Ndio – nafahamu kuwa huwezi kuelewa . lakini ujue kwamba mimi na mama yangu tunazungumza. Mama yangu ameweka mambo mengi wazi. Angalia, Des! Anakutana na vijana wengi wanaokuja katika kliniki kila siku, wana watoto ambao hawakupanga kuwapata, Des – Hii ni kwa sababu wasichana wengi huwa hawajui kitakachotokea wanapofanya mapenzi na wavulana wao.

26. DESIREE: Nyanya yangu anasema kuwa msichana lazima ajichunge mpaka atakapo olewa.

27. LORRAINE: Ndio , naheshimu wazo hilo, lakini Sazi na mimi uhusiano wetu ni wa dhati na tuko pamoja kwa mwaka mzima sasa. Dada yako Bella, anaishi na mpenzi wake pia. Ikiwa hapati mimba basi bila shaka anatumia njia fulani ya kupanga uzazi.

28. DESIRÉE: Labda. Sijawahi kufikiri juu ya hilo.

29. LORRAINE: sasa basi hakuna maswali zaidi. Tuendelee na mazoezi ya kuimba! There's Tuna kazi ngumu!

30. **SFX:** Lorraine and Desirée go through the new song again.

**NARRATOR:** Usiku mzuri! Des amelala kwenye shuka safi nyeupe huku akiwaza je dada yake atasema nini atakapo muuliza mbona hajapata mtoto mpaka sasa. Hata hivyo alipitiwa na usingizi mnono na alipoamka asubuhi ya pili alidhani atamsikia mdogo wake Endurance akiwapigia uluzi ng'ombe, au atawasikia majogoo wakiwika. Lakini asubuhi hii badala ya kusikia sauti za shamba katika kijiji cha Mtelera, alisikia sauti za magari katika mji wa Kentown, na kwa mbali alisikia mlio wa king'ora cha gari la wagonjwa au labda gari la polisi? Hapo alikwenda jikoni na kuwakuta Lorraine na nduguye pacha, Eric, tayari wameamka na wanatengeneza chai na mkate wa tosti.

<u>**Scene 2 in the kitchen at Aunty Alice's house**</u>

31. **SFX:** Kitchen sounds. Early morning. City sounds in background.

32. ERIC: Habari za asubuhi Desirée. Mbona umeamka mapema. Najua ni mafunzo kuwa ni lazima uamke mapema ! je umelala vyema?

33. DESIRÉE: Vyema sana, asante.

34. ERIC: karibu – mkate wa tosti na jamu.

35. DESIRÉE: Asante sana. (chewing)

36. ERIC : Des lazima niseme. Una sauti nzuri sana ya kuimba. Jana usiku ilifikia mahali ikawa nashindwa kutafautisha sauti yako na wimbo katika CD!

37. DESIRÉE: (laughing) Unanitania sio?

38. ERIC: No! Seriously! You will have to think hard about your future with a voice like that.

39. DESIREE: Oh? What do you mean?

40.

41. ERIC: Loo! – waweza kuacha shule uwe pop idol utapata mamilioni au unaweza kwenda college na muziki ukauweka kwa ajili ya baadae.

42. DESIRÉE: (laughing)Oh yote ni bure tu! Ningependa kuwa mwimbaji lakini siwezi kuondoka nyumbani hadi watoto wa mjomba Blessing watakapo kuwa wakubwa. kwahivyo –

(sounding cheery) nachukua jukumu la mama wa nyumbani kabisa.

43. ERIC: hapana, Des – usiyahini maisha yako namna hiyo!

44. DESIRÉE: kwani huko ni kuyahini maisha yangu? Hivyo ndivyo mama yangu alivyofanya.

45. ERIC: lakini nafikiri mama yako alijutia kuacha shule akiwa na umri mdogo. Hivyo ndivyo alivyomwambia mama yangu.

46. DESIRÉE: (thoughtfully) Ni kweli. Lakini...mimi, Sidhani kama nitaweza kwenda college.

47. ERIC: Nadhani unajua kwamba kuna fedha za msaada wa masomo kwa wanafunzi walio na maksi nzuri. Ni lazima ulifanyie bidii jambo gumu unalolitaka, hiyo ni changamoto – Hebu jifikirie utakuwa wapi katika kipindi cha miaka kumi ijayo?

48. DESIRÉE: (getting upset) Sikiliza Eric – ni vigumu kwangu kuweza kupanga mipango sasa hivi . Mama yangu amefariki, Shangazi yangu pia amefariki na mimi ndio nabeba jukumu

| | | |
|---|---|---|
| | | la kuwalea binamu zangu wanne wadogo pamoja na mdogo wangu, Endurance. |
| 49. | ERIC: (quietly) | Samahani. Sikuwaza hilo. Kwani mjomba wako yuko wapi? |
| 50. | DESIRÉE: | Yuko Granville. Alisema amekwenda kutafuta kazi na mke mwingine halafu atarudi kuwachukua watoto wake. |
| 51. | ERIC: | Basi labda anahitaji kukumbushwa. |
| 52. | **SFX:** toast/plates/cups | |
| | | Hey! Ongeza chai. |
| 53. | DESIRÉE: | asante. Baba yangu pia yuko huko. Alisema tunaweza kwenda kumtembelea lakini hata hajarudi nyumbani mpaka leo. Hata sijui yuko upande gani wa mji huo wa Granville. |
| 54. | ERIC: | Wajua? Hata mimi baba yangu amehamia katika mji wa Granville kwa sababu za kikazi. Twaweza kwenda kukaa kwa baba yangu halafu tuwatafute babako na mjombako, sidhani kama itakuwa kazi ngumu. |

55. DESIRÉE: (dreamily) Tukakae Granville? Halafu tumtafute baba yetu? Oh Eric! Endurance atafurahi sana. Anamtamani sana baba. Oh! Saa zimepita. Inabidi nimshtue Lorraine. Tuna miadi na Bongo saa sita, Tutaimba. Halafu saa tisa tutapanda basi mjini na Endurance.

56. ERIC: Sikiliza, Des. Kaa kidogo usiwe na haraka mimi ninaweza kuwapeleka kwa gari wewe na Endurance baadae. Hivyo utaweza kunieleza mashindano yalikwendaje. Unasemaje?

MUSIC UP

57. **NARRATOR:**

Desirée alikubali. Saa sita kamili Desirée na Lorraine walipiga kengele kwenye mlango wa ofisi ya Rainbow. Walifanya mazoezi kwa bidii – na sasa ni wakati wa kuimba mbele ya Bongo. Je atavutiwa na sauti zao?

58. **SFX:** SONG WITH FRENCH AND ENGLISH

*Je t'aime. Tu m'aimes. We're similar but not the same.*
*I do the things you want me to do*
*But is it because I love you?*

*Je t'aime. Tu m'aimes, but we don't love the same.*
*I say no, but you say Babe, then show me*
*How else can I  know.*

**Scene 3  In Studio**

59. **SFX:** Lorraine and Desirée singing. Clapping.

60. BONGO: Wow, wasichana – kuna matumaini kwenu! Tena makubwa! Na wewe, Des – una sauti maridadi – nzuri sana.

61. LORRAINE: Je tuliimba vizuri?umezionaje sauti zetu?

62. BONGO: Lorraine – una kipaji. Na wewe, Des! angalieni! Mimi ni mfanya biashara wa uhakika. Najua kipawa punde tu nikiona. Nyinyi ni wadogo bado, mna  umri gani?

63. DESIRÉE: Mimi nina miaka16.

64. BONGO: Sawa sawa ? kwa hivyo umepita. Nina hakika naweza kukutegemea. Tumebaki na mwezi mmoja kabla ya mashindano ya kuchagua vipawa kufanyika. Tatizo ni kwamba hamuwezi kushiriki pamoja na pia nina uwezo wa kumshughulikia mmoja wenu tu katika show hii ijayo. Ninahitaji

kuchagua sauti zingine pia. Hebu niwarekodi kila mmoja peke yake halafu nitawapigia simu nikisha pitisha uamuzi.

65. DESIRÉE: Mimi sina simu.

66. BONGO: Chukua hii hapa. Ina muda wa kutosha wa maongezi! Chukua!

**NARRATOR:** Lorraine alijiamini. Kwasababu Bongo alimfahamu kwa muda mrefu. Kwa hivyo alikuwa na uhakika kuwa yeye ndie atakaechaguliwa. Njiani wakielekea Mtelera Eric alimtia moyo Desirée alimsihi asikate tamaa. Walipofika walibaki ndani ya gari wakizungumza kwa karibu saa nzima. Mwishowe nyanya alitoka nje na kumwita mjukuu wake. Eric aliondoka lakini baada ya kuinakili namba mpya ya simu ya Desirée. Baadae kila mtu alipokuwa amelala, Desirée alikwenda nje chini ya miembe ili kumweleza mama yake.Kadri upepo ulivyo zidi kuvuma nae alifunika zaidi khanga yake huku akiimba nyimbo aliyoipenda mama yake, lakini mara hii aliimba kwa ajili ya Eric.

(Signature tune up)

**OUTRO.**

Na huo ndio mwisho wa sehemu hii ya nne ya mchezo wa kusisimua katika Noa Bongo Jenga maisha Yako,. Usikose kujiunga nasi katika sehemu ya tano ya mchezo Chini Ya Miembe ambapo Lorraine na dada yake Desirée, Bella, wanalikabili swala la kuzuia mimba zisizo

takikana.Kumbuka unaweza kuusikiliza tena mchezo huu pia mwambie rafiki yako juu ya hadithi hizi za kusisimua. Anwani yetu ya mtandao ni dw- world . de mkwaju lbe Hadi wakati mwingine kwaheri.

**END OF EPISODE FOUR**